BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2017

021 KISWAHILI

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2017

021 KISWAHILI

Kimechapishwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO

DIBAJI iv

1.0 UTANGULIZI 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI 2

2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO 2

2.1.1 Swali la 1: Ufahamu 2

2.1.2 Swali la 2: Ufupisho 7

2.2 SEHEMU B: SARUFI 10

2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno 10

2.2.2 Swali la 4: Matumizi ya Kamusi 12

2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA 15

2.3.1 Swali La 5: Dhima za Lugha 15

2.3.2 Swali la 6: Maana na Matumizi ya Misimu 17

2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA 21

2.4.1 Swali la 7: Fasihi Simulizi 21

2.4.2 Swali la 8: Fasihi Simulizi 24

2.4.3 Swali la 9: Fasihi Simulizi 26

2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI 31

2.5.1 Swali la 10: Uandishi wa Insha 31

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KATIKA MADA 36

4.0 HITIMISHO 37

KIAMBATISHO A 39

KIAMBATISHO B 40

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa kufaulu katika upimaji huo kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera na wadau wa elimu kwa jumla.

Taarifa hii ni tathmini ya kati inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Kimsingi uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu unalenga kuonesha dhahiri maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha Sekondari, Kidato cha Kwanza na cha Pili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za wanafunzi kufanya vizuri, vibaya au kwa kiwango cha wastani katika maswali/mada mbalimbali zilizopimwa. Baadhi ya sababu zilizofanya wanafunzi kufanya vizuri ni kama vile kuwa na uelewa mzuri wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya swali. Sababu za wanafunzi kuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu zimeelezwa kuwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojitosheza. Aidha, sababu zilizofanya wanafunzi wachache kutopata alama za juu katika majibu yao zimefafanuliwa kama vile kutoelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa kuelezea dhana mbalimbali kwa ufasaha na udhaifu katika kuelewa dhana zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa jumla. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika upimaji ujao utakaotolewa/kuendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania linakaribisha maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha ripoti zitakazofuata.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani na walimu wa somo waliohusika katika kutayarisha ripoti hii. Tunapenda vilevile kutoa shukrani zetu za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Utafiti Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika ripoti hii.

Dr. Charles Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili mwaka 2017 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali katika upimaji wa somo la Kiswahili. Upimaji huu ulikuwa na maswali kumi (10) yaliyogawanywa katika sehemu A (Ufahamu), B (Sarufi), C (Mawasiliano na Utumizi wa Lugha), D (Fasihi kwa Ujumla) na E (Uandishi wa Insha/Utungaji). Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu A hadi E.

Upimaji wa Kiswahili Kidato cha Pili mwaka 2017 ulifanywa na jumla ya wanafunzi 485,532 kati ya wanafunzi 521,064 walioandikishwa ambapo wavulana ni 231,513 na wasichana ni 254,019. Katika upimaji huo, wanafunzi waliofaulu ni 445,496 sawa na asilimia 91.92. Kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi kwa jumla katika upimaji huu kilikuwa cha juu kwa asilimia 1.86 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2016 ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa ni asilimia 90.06.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na yale yaliyojibiwa vibaya katika upimaji kinyume na matarajio ya wanafunzi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni *vizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha kufaulu kimeanzia alama 65 hadi 100, kiwango cha wastani kikianzia alama 30 hadi 64 na kiwango hafifu alama 0 hadi 29. Aidha, chati mbalimbali zimewekwa ili kufafanua viwango hivyo vya kufaulu kwa wanafunzi ambapo rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya njano inawakilisha kiwango cha wastani na rangi nyekundu ikiwakilisha kiwango hafifu cha kufaulu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na wanafunzi.

Kwa jumla, uchambuzi huu utaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO

2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilihusu *Ufahamu* ambapo wanafunzi walipaswa kusoma kifungu cha habari na kisha kujibu maswali yaliyofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa wanafunzi.

> *Tafiti zilizofanyika zinaonesha kuwa asilimia sitini ya raia wa mataifa yanayoendelea wanaishi katika hali ya umasikini. Kwa mujibu wa maelezo ya tafiti za Umoja wa Mataifa, watu masikini pato lao ni chini ya dola moja kwa siku. Uchumi wa mataifa hayo hutegemea sana kilimo ambacho huendeshwa kwa kutegemea mvua, ambayo kwa bahati mbaya mara kwa mara huwa* ***adimu****.*
>
> *Yapo mataifa ambayo yametatua tatizo la ukosefu wa mvua kwa kutumia miradi ya umwagiliaji maji kutoka katika mito na maziwa. Miradi hii huhakikisha kuwa harakati za kilimo hazitegemei mvua pekee. Suala la umwagiliaji linahitaji uwekezaji mzuri na utengaji wa* ***kasma*** *ili kugharamia miradi yenyewe ambayo inaweza kuwa* ***ghali****. Uwekezaji huu unaweza kuwapo ikiwa viongozi wataweka msisitizo katika miradi husika.*
>
> *Katika mataifa mengine kuna juhudi za kuhakikisha kuwa maji ya mvua yanahifadhiwa katika njia ifaayo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na hata katika umwagiliaji mashambani. Maji hayo yanaweza kuhifadhiwa kwa utengenezaji wa mabwawa. Isitoshe uchimbaji wa visima vya maji unaweza kusaidia pia.*
>
> *Licha ya kuwa maji yatokanayo na visima hayawezi kutumika katika umwagiliaji kwa kiwango cha juu, maji hayo yanaweza kutumika katika kilimo cha bustani. Kilimo cha namna hii kinaweza kupunguza* ***adha*** *ya maisha kwa wananchi.*

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima ufahamu wa mwanafunzi kwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na liligawanyika katika vipengele vinne yaani (a) hadi (d).

Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kuandika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hiyo na kisichozidi maneno matano. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kueleza kwa nini anadhani kuwa kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika. Kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kutaja njia tatu zinazotumiwa na baadhi ya nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua na kipengele (d) kilimtaka mwanafunzi aeleze maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Swali hili lilijibiwa vizuri na idadi kubwa ya wanafunzi waliopimwa. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 1: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Asilimia 74.76 ya wanafunzi hao walipata alama za wastani na zaidi. Miongoni mwao, wanafunzi wengi (54.25%) walipata alama za wastani 3 hadi 6 na wengine (20.51%) walipata alama za juu 6.5 hadi 10. Wanafunzi waliokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu waliweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi na kushindwa vipengele vichache. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu vizuri vipengele (a) hadi (c) kwa kuweza kuandika kichwa cha habari kinachofaa, kueleza sababu za kilimo cha umwagiliaji kuwa ni cha hakika na kutaja njia zinazotumiwa na mataifa yaliyoendelea katika kukabili uhaba wa mvua kwa usahihi na kushindwa kujibu kipengele (d) pekee kwa kutoa maana za maneno zisizowiana na habari na kupata alama za wastani. Kielelezo 1.1 kinaonesha sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kipengele (d).

Kielelezo 1.1

(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Adimu...Mataifa ambayo yametatua tatizo...

(ii) Kasma...Kugharamia miradi yenyewe ambayo ina weza kuwa ghali...

(iii) Ghali...Msisitizo katika miradi huisika...

(iv) Adha...Ni maisha kwa wananchi...

Kielelezo 1.1 kinaonesha sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyeandika maana za maneno kinyume na jinsi yalivyotumika katika habari na kupata alama 0 katika kipengele hicho.

Aidha, wanafunzi waliopata alama za juu katika swali hili waliweza kujibu vipengele karibu vyote kwa usahihi. Waliandika kichwa cha habari kulingana na maudhui halisi ya habari yaani "Kilimo cha Umwagiliaji" katika kipengele (a), kipengele (b) walieleza ni kwa nini kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika, kipengele (c) walitaja njia tatu zinazotumiwa na baadhi ya nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua ambazo ni kutumia maji ya mito, mabwawa na kuchimba visima virefu na katika kipengele (d) walieleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari waliyoisoma. Kielelezo 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele (a) hadi (d).

Kielelezo 1.2

Maswali

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyoisoma kisichozidi maneno matano.

KILIMO CHA UMWAGILIAJ

(b) Kwa mujibu wa habari uliyosoma unadhani ni kwa nini kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika?

Kilimo cho Umwagiliaji ni cho Uhakika kwa sababu Watu tena hawategemei sana Mvua kwa Mfano nchi Za Wenzetu huwama mirachi ya Umwagiliaji kubka kubka mito Mabwawa na Visima

(c) Taja njia tatu zinazotumiwa na baadhi ya nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua.

(i) mito mirachi ya maji kubka kwenye mito

(ii) Mabwawa Mirachi ya maji kubka kwenye Mabwawa

(iii) Visima Mirachi ya maji kubka kwenye Visima

(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Adimu Ni kitu ambacho cyo rahisi kupatikana Mara kwa mara

(ii) Kasma ni kiasi cho fecha kinachotenguwa ili ku fanya shughuli mbalimbali za kijamii

(iii) Ghali ni kitu ambacho kinauzwa kwa elo ku bwa

(iv) Adha ni vitu vinayotuzeza kama kipindi fulani cha maisha

Kielelezo 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kutoa majibu sahihi katika vipengele vyote vya swali ijapokuwa alikuwa na matatizo ya kiundishi katika kipengele (a) ambapo herufi ‘I’ imeachwa kwenye neno UMWAGILIAJI, (d) (iii) ambapo aliandika neno “ela” badala ya hela. Pia uandishi wake wa herufi kubwa na ndogo hauleweki hususan herufi ‘m’ na ‘k’ hazieleweki zinapokuwa kubwa au ndogo katika sentensi zake.

Kwa upande mwingine, asilimia 25.24 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walifaulu kwa kiwango hafifu kutokana na kushindwa kujibu maswali katika vipengele vingi. Miongoni mwao, wanafunzi 33,978 sawa na asilimia 6.99 walipata 0 kutokana na kushindwa kujibu vipengele vyote. Wanafunzi hao hawakuweza kuandika (a) kichwa cha habari kwa usahihi, (b) kutoa sababu kwa nini kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika, (c) kutaja njia tatu zinazotumiwa na baadhi ya nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua na (d) walishindwa kabisa kueleza maana ya maneno waliyopewa kama yalivyotumika katika habari. Kielelezo 1.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu vipengele vyote ambapo katika kipengele (c) alitaja maneno *Adimu*, *Kasma*, na *Ghali* kama njia tatu zinazotumiwa na nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 1.3

Maswali

(a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyoisoma kisichozidi maneno matano.

Wanaishi katika hali ya umwagiliaji.

(b) Kwa mujibu wa habari uliyosoma unadhani ni kwa nini kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika?

Maji hayo yanaweza kuhifadhiwa kwa Utengenezaji wa mabwawa. Isitoshe maji ya mvua ~~yata~~ yanahifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

(c) Taja njia tatu zinazotumiwa na baadhi ya nchi zinazoendelea katika kutatua tatizo la uhaba wa mvua.

(i) Adimu

(ii) Kasma

(iii) Ghali



(d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma.

(i) Adimu...uchumi wa mataifa hayo hutegemea sana kilimo-ambacho huendeshwa kwa kutegemea mvua ambayo kwa bahati mbaya.

(ii) Kasma...ni...Sucala la umuagilaji linahitaji uwekezaji mzuri.

(iii) Ghali...Uwekezaji huu unaweza kuwepo lkiwa Viongozi watawaka msisitiza ktk mgradi husika.

(iv) Adha...hilimo cha namna hii kinaweza kupunguza-kasi ya maisha kuea uananchi.

Kielelezo 1.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi ambaye hukuweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote.

2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kutumia maarifa ili kufupisha habari waliyoisoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5 na lilimtaka mwanafunzi kufupisha habari kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60). Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi waliofanya upimaji huu. Asilimia 70.14 ya wanafunzi hao walifaulu kwa kiwango kizuri (cha juu) na cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu kwa wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 2: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Idadi kubwa ya wanafunzi (62.77%) walifaulu kwa kiwango cha wastani na kupata alama 1.5 hadi 3 kutokana na kuandika ufupisho usiojitosheleza kwa kuzingatia baadhi tu ya mambo muhimu katika ufupisho wa habari kama vile kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha maana, kuwa na mtiririko wenye mantiki, kuzingatia wazo kuu la habari na idadi ya maneno. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika ufupisho bila kuzingatia wazo kuu la habari na idadi stahiki ya maneno na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi wa aina hiyo.

Kielelezo 2.1


2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60)

U maskin ni kitu ambayo imetokea katika nchi yetu kwasababu ya uchumi wa mataifa hayo hutegemea sana kilimo cha utegemeziya mvua: katika mataifa nyingina kuna juhudi zakutakisha kuwa maji ya mvua ni muhimu. katika kunyay kwashavyomba, kwa i ya nyumbani

Kielelezo 2.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari kwa kutumia maneno yake mwenyewe lakini hakuzingatia mawazo makuu ya habari na idadi ya maneno. Aidha, mwanafunzi huyu alikuwa na tatizo la kisarufi hasa katika muundo wa tungo kama vile “utegemezi ya mvua” badala ya utegemezi wa mvua.

Wanafunzi waliofaulu kwa kiwango cha juu walikuwa ni wachache yaani asilimia 7.37 pekee ndio waliopata alama 3.5 hadi 5. Miongoni mwao, asilimia 0.51 waliandika habari kwa kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha maana, kuzingatia mawazo makuu na yenye mpangilio unaoleta mantiki, uzingatiaji wa idadi ya maneno bila kupotosha kiini cha habari ya awali na kupata alama zote 5. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika ufupisho kwa kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari ya awali na kupata alama zote.

Kielelezo 2.2


2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).

Watu wengi katika nchi zinazpendelea wamekumbwa na umaskini kwa sababu ya kutegemea kilimo cha mvua ambao si ya mara kwa mara. Mataifa mengine wameendelea kwa sababu wametatua tatizo hilo kwa kuhakikisha wanachi hawategemei mvua hivyo wameanzisha mradi wa umwagiliaji wa maji kutoka kwenye mito, pia wamehifadhi maji ya mvua kutengeneza mabwawa na kudimba visima (54)

Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika ufupisho uliozingatia wazo kuu la habari, kutumia maneno yake mwenyewe na kutumia idadi stahiki ya maneno (54).

Pamoja na kiwango kizuri cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili, wanafunzi wachache (29.86%) walipata alama 0 hadi 1 kwa kuwa hawakuzingatia kanuni za uandishi wa ufupisho kama vile; kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari ya awali, kuzingatia mtiririko wa mawazo wenye mantiki, kuzingatia taratibu za uandishi, matumizi ya lugha sanifu na kuzingatia idadi ya maneno kama ilivyotakiwa. Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu swali hili kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 2.3


2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).

Tafiti uliozianzika zinaonyesha kuwa asilimia sitini ya raia wa mataifa yanayoendelea wanaishi katika hali ya umaskini. Kwa mujibu wa maelezo ya tafiti za umoja wa mataifa, watu maskini pale lacini chini ya dola moja kwa siku. Haya mataifa ambayo yametatua tatizo la ukosefu wa mvua kwa kutumia miradi ya kilimo cha umwagiliaji-

Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kutumia maneno yake mwenyewe na badala yake kunukuu aya ya kwanza katika habari aliyopewa kinyume na matakwa ya swali.

2.2 SEHEMU B: SARUFI

2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na mada ndogo ya *Uambishaji*. Swali lilimtaka mwanafunzi kueleza dhima mbili kwa kila mofimu iliyopigiwa mstari katika maneno aliyopewa katika sentensi (a) hadi (e). Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutumia maarifa katika kubainisha dhima za mofimu na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya na wanafunzi wengi ambapo asilimia 86.28 walifaulu kwa kiwango hafifu ambapo ni asilimia 13.72 pekee ndio waliojibu swali hili na kufaulu kwa kiwango cha wastani na cha juu. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 3: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Wanafunzi wengi (86.28%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango hafifu kwa kupata alama 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kueleza dhima za mofimu walizopewa. Aidha, wanafunzi hao walikosa uelewa wa kutosha kuhusu dhima za mofimu na wengine hawakuwa na maarifa yoyote kuhusu mofimu na dhima zake kwa jumla kama vile kudokeza nafsi, hali ya umoja na wingi wa nomino, urejeshi, hali ya usababishi, hali ya ukanushi, mtendwa na kuonyesha njeo mbalimbali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kabisa kueleza dhima za mofimu zilizopigiwa mistari kwa kuandika maana ya sentensi hizo kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyefafanua sentensi alizopewa isivyo, badala ya kuelezea dhima za mofimu zilizopigiwa mstari katika sentensi hizo.

Kielelezo 3.1



3. Eleza dhima mbili kwa kila mofimu iliyopigiwa mstari.

(a) Mama atakuja kesho.

Mama atakaja kesho yani nimtu anaye simuka na mwenzi na kusema mama anakaja kesho

(b) Mti umeanguka.

Ni mti wa muda mrefu umekaa na Muzisho wake kukauka na kuona na kuanguka

(c) Mwalimu alimfundisha Juma.

Mwalimu alingia darasani na ku mfundisha Juma peke yake wengine akawacha.

(d) Ninakupenda.

Ni mtu aliye ongea na mwenzie na kumwambia anampenda sana.

(e) Sitakuja shuleni kesho.

Hatakuja Shuleni Kesho kwa agili ya ma tatizo mbalimbali

Kielelezo 3.1 kinadhirisha majibu ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuelezea dhima za mofimu zilizopigiwa mstari kama atakuja (wakati ujao/hali ya kutarajia), umeanguka (idadi/kiambishi jina), alimfundisha (nafsi/idadi), ninakupenda (nafsi/idadi/mtendwa) na sitakuja (ukanushi/nafsi) kwa kutoa maelezo ya kufafanua sentensi zilizo na mofimu hizo kinyume na matakwa ya swali.

Kwa upande wa wanafunzi waliojibu vizuri swali hili, asilimia13.29 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3 hadi 6 kwa kuwa walieleza dhima sahihi kwa baadhi ya mofimu na kushindwa kuelezea mofimu nyingine. Wanafunzi wachache sana (2,069) sawa na asilimia 0.43 walifaulu kwa kiwango cha juu kwa kupata alama 6.5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kueleza dhima za mofimu walizopewa kwa usahihi. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za juu za kwa kujibu kwa usahihi vipengele (c), (d) na

(e) kwa usahihi japokuwa katika vipengele (a) na (b) alieleza dhima moja tu badala ya mbili.

Kielelezo 3.2



Eleza dhima mbili kwa kila mofimu iliyopigiwa mstari.

(a) Mama atakuja kesho.

i) Huonesha jambo hilo litatendeka wakati ujao

ii) Huonesha urejeshi

(b) Mti umeanguka.

i) Huonyesha idadi ya wahusika (Mhusika ni mmoja)

ii) Huonyesha urejeshi

(c) Mwalimu alimfundisha Juma.

i) Kuonyesha nafsi ya tatu umoja

ii) Kuonyesha urejeshi

(d) Ninakupenda.

i) Huonesha nafsi ya pili umoja

ii) Kuonyesha urejeshi

(e) Sitakuja shuleni kesho.

i) Huonesha ukanushi / hali ya kutokanusha

ii) Huonyesha nafsi ya kwanza umoja

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetoa majibu sahihi kwa kueleza dhima za mofimu kulingana na matakwa ya swali ijapokuwa alikuwa na upungufu katika kipengele (a) na (b) ambako alieza dhima moja tu sahihi kwa kila kipengele badala ya dhima mbili kama ilivyotakiwa.

2.2.2 Swali la 4: Matumizi ya Kamusi

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za Maneno* katika mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mwanafunzi kupanga maneno aliyopewa kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi na lilikuwa na jumla ya alama 10. Wanafunzi wengi waliojibu swali hili walifanya vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na

cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu katika asilimia.



Chati Na. 4: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 87.89 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walipata alama za wastani na zaidi. Wanafunzi wengi kati ya hao (79.79%) walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kupanga kwa usahihi maneno waliyopewa kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi. Kiwango hiki kizuri cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili kinadhihirisha kuwa mada ndogo ya *Matumizi ya Kamusi* ilieleweka vizuri kwa wanafunzi wengi. Hata hivyo, wanafunzi wachache (8.1%) walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa kupata alama 3 hadi 6 kutokana na kukosea kupanga baadhi ya maneno kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika neno “Anzali” kabla ya Adhabu na “Duwaa” kabla ya Dabiri na hivyo kupata alama 6. Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kupanga maneno yote kumi kama yanavyotakiwa yawe katika kamusi na kupata alama zote.

Kielelezo 4.1

4.	Panga maneno yafuatayo kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi.		
	(a)	Duwaa	(a) Adhabu
	(b)	Chichiri	(b) Anzali
	(c)	Adhabu	(c) Chege
	(d)	Kidahizo	(d) Chichiri
	(e)	Faladi	(e) Dabiri
	(f)	Chege	(f) Duwaa
	(g)	Kitomeo	(g) Faladi
	(h)	Dabiri	(h) Fanusi
	(i)	Anzali	(i) Kidahizo
	(j)	Fanusi	(j) Kitomeo

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kupanga maneno aliyopewa kutoka kipengele (a) hadi (j) kwa usahihi.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (12.11%) waliojibu swali hili walipata alama za chini 0 hadi 2.5 na kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa sababu baadhi yao walichanganya maneno hayo kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha ya kupanga maneno katika kamusi. Miongoni mwao, asilimia 8.82 walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na maarifa yoyote kuhusu mpangilio wa maneno katika kamusi na hivyo kupanga maneno bila mtiririko unaotakiwa. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kupanga maneno kwa kuanza na yenye herufi ‘Ch’ ikifuatiwa na ‘D’, ‘F’, ‘K’, na kumalizia na herufi ‘A’ kinyume na mpangilio halisi wa maneno katika kamusi.

Kielelezo 4.2

4. Panga maneno yafuatayo kama yanavyotakiwa kuwa katika kamusi.

(a)	Duwaa	(a)	Chege
(b)	Chichiri	(b)	Chichiri
(c)	Adhabu	(c)	Dabiri
(d)	Kidahizo	(d)	Duwaa
(e)	Faladi	(e)	Faladi
(f)	Chege	(f)	Fanusi
(g)	Kitomeo	(g)	Kidahizo
(h)	Dabiri	(h)	Kitomeo
(i)	Anzali	(i)	Adhabu
(j)	Fanusi	(j)	Anzali

Kielelezo 4.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyepanga maneno bila kuzingatia utaratibu wa kupanga maneno katika kamusi na kupata alama 0.

2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

2.3.1 Swali La 5: Dhima za Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Mawasiliano* na mada ndogo ya *Lugha kama Chombo cha Mawasiliano* na lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali lililenga kupima maarifa na lilimtaka mwanafunzi kueleza kwa kifupi dhima tano za lugha katika jamii. Swali hili pia ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi. Jedwali Na. 1 linaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.

Jedwali Na. 1: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya wanafunzi
0 - 2.5	154,300	31.70
3 - 6	245,248	50.45
6.5 - 10	86,763	17.85

Asilimia 68.3 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walifaulu kwa viwango vizuri na vya wastani. Hata hivyo, wanafunzi wengi zaidi (50.45%) walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa sababu walikuwa wanachanganya baadhi ya majibu yao na dhima za fasihi pamoja na dhima za lugha katika jamii. Wanafunzi wengine walitaja hoja bila ya kutoa maelezo ya kutosha katika hoja husika na hivyo kupata alama za wastani. Wanafunzi waliojibu vizuri na kupata alama za juu katika swali hili walikuwa ni asilimia 17.85 ambao waliweza kueleza kwa kifupi dhima tano za lugha katika jamii kama *chombo cha mawasiliano, chombo cha kutoa mafunzo/maonyo, chombo cha kuendeleza utamaduni wa jamii, kitambulisho cha jamii na chombo cha kuendeleza umoja na ushirikiano* na kupata alama za juu 6.5 hadi 10. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeeleza kwa kifupi dhima za lugha kama ilivyotakiwa.

Kielelezo 5.1


5. Eleza kwa kifupi dhima tano za lugha katika jamii.

(a) Lugha ni utambulisho wa jamii. Kwa mfano Watanzania hutambulishwa kwa lugha ya Kiswahili.

(b) Lugha ni nyenzo ya Kudhihirisha hisia, kwa mfano lugha ya ukali hutumiwa na mtu aliyekasirika

(c) Lugha huelimisha. Lugha hutumika kuwapa watu mafunzo mbali mbali ya maisha.

(d) Lugha huendeleza utamaduni wa jamii. mfano Wazee wanotamba hadithi kwa wajukuu zao.

(e) Lugha huwawezesha watu kuwasiliana,hii ni kwa njia ya kupashana habari baina ya watu.

Kielelezo 5.1 kinadhihirisha jibu la mwanafunzi aliyeweza kueleza kwa usahihi dhima za lugha katika jamii kama swali lilivyotakiwa ijapokuwa hoja ya ‘mawasiliano’ na ‘kudhihirisha hisia’ ni hoja zenye dhima moja.

Aidha, baadhi ya wanafunzi (31.7%) walipata alama hafifu 0 hadi 2.5 kwa kuwa walishindwa kueleza hoja zao kama zilivyotakiwa, huku wengine wakiandika dhima za fasihi badala ya dhima za lugha katika jamii kama ilivyotakiwa iwe. Wanafunzi wengine (10.48%) katika

kundi hili walipata alama 0 kwa kuwa walikuwa hawana maarifa kabisa kuhusu dhima za lugha na hivyo kuandika sentensi kama *kuifanya jamii kuwa vizuri katika maendeleo* na nyinginezo zisizowiana na dhima za lugha katika jamii kama kielelezo 5.2 kinavyodhihirisha majibu hayo yasiyo sahihi.

Kielelezo 5.2


5. Eleza kwa kifupi dhima tano za lugha katika jamii.

(a) Kuelimisha jamii

(b) Kusaidia watu wakiwa wanaongea

(c) kukuza jamii

(d) kuifanya jamii kuwa kizuri katika maendeleo

(e) lugha ni sauti za watu zinazotumiwa na binadamu.

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza dhima za lugha kutoka kipengele (a) hadi (e).

2.3.2 Swali la 6: Maana na Matumizi ya Misimu

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha mbalimbali* na lililenga kupima maarifa. Swali lilikuwa na vipengele (a) na (b) na lilikuwa na jumla ya alama 10. Kipengele (a) kilimtaka mwanafunzi kueleza maana ya misimu katika lugha ya Kiswahili na kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi kufafanua sifa nne za misimu. Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili katika asilimia.



Chati Na. 5: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Aidha, wanafunzi wengi (57.60%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu (cha chini) cha kufaulu kutokana na kushindwa kueleza maana ya misimu na kufafanua sifa za misimu isivyo na kupata alama 0 hadi 2.5. Karibu nusu ya wanafunzi hao, asilimia 25.3, walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu mada ndogo ya *Misimu katika Lugha ya Kiswahili*. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alieleza maana ya misimu kama "aina ya neno (kivumishi)" badala ya kuelezea kama;

> maneno yasiyo sanifu yanayozushwa na kikundi cha watu wachache wenye utamaduni mmoja na ambayo huweza kuingizwa katika lugha sanifu yanapotumiwa kwa muda mrefu.

Aidha, mwanafunzi huyu alifafanua sifa za misimu kwa kuonesha aina za misimu kama vile *zagao*, *tarafa* na *endelevu* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kueleza maana ya misimu na pia hakuweza kufafanua sifa za misimu kama swali lilivyotaka.

Kielelezo 6.1



6. (a) Eleza maana ya misimu katika lugha ya Kiswahili.

Musimu ni aina ya maneno au ni neno ambalo hutumika kwa kuumishwa ambalo linaweza likatu, mika kwa muda na baadae kupotea

(b) Fafanua sifa nne za misimu.

(i) Misimu huwa ni zagao misimu zagao ni misimu ambayo inaweza kuzagaa katika mji

(ii) Misimu tarafa ni misimu ambayo huenea katika tarafa

(iii) Pia kuna baadhi ya misimu ambayo hu zagaana kupotea

(iv) Pia kuna misimu endelevu baadhi ya maneno ya misimu huwa ni ya kudu mu

Kielelezo 6.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kueleza maana ya misimu na kushindwa kufafanua sifa za misimu badala yake akaandika aina za misimu kama *zagao, tarafa* na *endelevu* kinyume na matakwa ya swali.

Asilimia 42.4 ya wanafunzi walipata alama za wastani na zaidi. Idadi kubwa ya wanafunzi (33.74%) walipata alama za wastani 3 hadi 6 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kueleza maana ya misimu na ufafanuzi kuhusu sifa za misimu. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kueleza maana ya misimu katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi lakini katika kufafanua sifa za misimu; mwanafunzi huyo alifafanua sifa mbili pekee kati ya sifa nne zilizotakiwa. Kielelezo 6.2

ni sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyefafanua baadhi ya sifa za misimu kwa usahihi huku akishindwa nyingine na kupata alama za wastani.

Kielelezo 6.2


(b) Fafanua sifa nne za misimu.

(i) Misimu huzuka na ~~kuto~~ kupotea kwa muda mfupi. Misimu ikizuka katika watu fulani isipotumiwa na watu wengi hupotea katika matumizi.

(ii) Kubadilika baada ya misimu mingine kuingia, misimu mbalimbali hubadilika misimu mingine ikingia mfano sasa watu hawatumii sana neno bambucha.

(iii) Misimu hupendwa sana na vijana, vijana mbalimbali hupenda kutumia misimu mbalimbali mfano Oya kijana toa kwingu hapa hatukutaki.

(iv) Misimu yenye kutumiwa kwa muda mrefu hupanda hadhi na kuwekwa katika msamiati ya lugha ya kawaida.

Kielelezo 6.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyefafanua sifa mbili za misimu kwa usahihi na kukosea sifa mbili.

Wanafunzi wengine katika kundi hili (8.66%) pekee, ndio waliojibu swali hili vizuri na kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kueleza maana ya misimu katika lugha ya Kiswahili na kufafanua sifa nne za misimu zilizozingatia *chanzo cha misimu, matumizi ya lugha isiyo sanifu, matumizi ya lugha ya mafumbo/yenye chuku nyingi* na jinsi *zilivyo na mvuto kwa jamii* kwa usahihi. Kielelezo 6.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kueleza maana na kufafanua sifa za misimu kama ilivyotakiwa.

Kielelezo 6.3



(a) Eleza maana ya misimu katika lugha ya Kiswahili.

Misimu ni lugha isiyosanifu inayozuka na kutoweka kwa muda mfupi na ile inayodumu hasanifiwa kwa muda mrefu husaniffiwa na kulifanya kuwa msamiati sahihi wa lugha.

(b) Fafanua sifa nne za misimu.

(i) Ni lugha isiyo sanifu.

Misimu ni lugha isiyo sanifu kwa sababu huzishwa na kikundi cha watu fulani na kutumika kumaanisha Jambo

(ii) Ni lugha ya mafumbo.

Misimu ni lugha ya mafumbo kwa sababu unaweza mwa watu ambala lakini wao
itakawa mengoni lakini wahataja neno hujawahi lisikia wanjua kimchoendele

(iii) Ina chuku (chumvi) nyingi.

Misimu ina chumvi nyingi kwa sababu mara nyingine huelezea Jambo la uongo.

(iv) Hupendwa na watu wengi

Misimu huwa na kawaida ya kupendeua na kutumika na watu wengi.

Kielelezo 6.3 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeeleza maana ya misimu vizuri na kufafanua sifa stahiki za misimu kwa kuzingatia matakwa ya swali.

2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA

2.4.1 Swali la 7: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lilikuwa na sehemu (a) na (b). Katika sehemu (a) mwanafunzi alitakiwa kutegua vitendawili kwenye vipengele (i) hadi (v) na katika sehemu (b) mwanafunzi alitakiwa kukamilisha methali zilizopo kwenye vipengele (i) hadi (v). Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.

Jedwali Na. 2: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya wanafunzi
0 - 2.5	28,137	5.79
3 - 6	218,971	45.04
6.5 - 10	239,036	49.17

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi na wanafunzi wengi. Asilimia 94.21 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walipata alama za wastani na zaidi na hivyo kulifanya swali hili kuwa na kiwango kizuri zaidi cha kufaulu. Kati yao, asilimia 49.17 walipata alama za juu 6.5 hadi 10. Hata hivyo wanafunzi (2.3 %) katika kundi hili walipata alama zote za swali kwa kuwa waliweza kutegua vitendawili na kukamilisha methali walizopewa kwa usahihi. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kutegua vitendawili na kukamilisha methali alizopewa kwa usahihi.

Kielelezo 7.1

7. (a) Tegua vitendawili vifuatavyo:

(i) Nasuka mkeka lakini nalala chini..Baga.....

(ii) Kila aendapo huacha alama..Konokono.....

(iii) Nikimpiga mwanangu watu hucheza..Ngoma:.....

(iv) Anatembea na nyumba yake...Kobe.....

(v) Nyumba yangu ina nguzo moja..Uyoga.....

(b) Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Vita vya panzi ..Furaha..ya...kunguni.....

(ii) Hakuna marefu ....Yaliyokuwa na naba.....

(iii) Siri ya mtungi ..aijuaye...kata.....

(iv) Baniani mbaya ..Kiatu chake...dawa.....

(v) Mgaagaa na upwa .hali...wali...mkavu.....

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kutegua vitendawili na kukamilisha methali alizopewa na kupata alama zote.

Hata hivyo, asilimia 45.04 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walipata alama za wastani kutokana na kushindwa kutegua baadhi ya vitendawili na kukamilisha baadhi ya methali ipasavyo kwa usahihi na hivyo kupata alama 3 hadi 6.

Licha ya swali hili kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, wapo wanafunzi wachache (5.79%) walioshindwa kutegua vitendawili na kukamilisha methali walizopewa kwa usahihi. Baadhi ya wanafunzi hao, wapo ambao hawakuelewa kabisa namna ya kutegua vitendawili na jinsi ya kukamilisha methali na hivyo kuandika maneno yasiyohusiana kabisa na dhana ya vitendawili au methali za Kiswahili na kupata alama 0. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kutegua vitendawili na kukamilisha methali alizopewa na hatimaye kutoa majibu yasiyowiana kabisa ama na vitendawili au methali.

Kielelezo 7.2

7. (a) Tegua vitendawili vifuatavyo:

(i) Nasuka mkeka lakini nalala chini..... Vifuatavyo

(ii) Kila aendapo huacha alama..... Usagali

(iii) Nikimpiga mwanangu watu hucheza..... hucheza

(iv) Anatembea na nyumba yake..... Siri ya mtungi

(v) Nyumba yangu ina nguzo moja..... nguzo moja

(b) Kamilisha methali zifuatazo:

(i) Vita vya panzi ..... mwanangu

(ii) Hakuna marefu ..... Siri ya marefu

(iii) Siri ya mtungi ..... mwanagu

(iv) Baniani mbaya ..... simulizi

(v) Mgaagaa na upwa ..... vifuatavya vya fani

Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kujibu vipengele vyote vya (a) na (b) na kupata alama 0. Aidha, mwanafunzi huyu aliandika maneno kama *usagali, hucheza*, …. kama majibu ya vitendawili kinyume na matakwa ya swali.

2.4.2 Swali la 8: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na lililenga kupima maarifa ya mwanafunzi katika kufafanua vipengele vya fani ambavyo ni; (a) Mandhari (b) Wahusika (c) Fanani (d) Hadhira na (e) Muundo. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa ni cha wastani. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.

Jedwali Na. 3: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya wanafunzi
0 - 2.5	204,371	42.02
3 - 6	188,312	38.73
6.5 - 10	93,457	19.23

Wanafunzi wengi (57.96%) walijibu vizuri na kupata alama za wastani na zaidi kwa kuwa wengi walionesha kuwa na uelewa wa vipengele vya fani katika uhakiki wa kazi za fasihi simulizi. Miongoni mwao, asilimia 38.73 walipata alama za wastani 3 hadi 6 kutokana na kushindwa kufafanua baadhi ya vipengele vya fani kwa usahihi hususani kipengele cha "fanani" ambacho wanafunzi wengi walikielezea kama "mtu anayetunga kazi za fasihi" badala ya kufafanua kuwa ni *mtoaji/mtambaji*, *msimuliaji/mtendaji* au *mwasilishaji wa kazi za fasihi simulizi.* Aidha, wanafunzi wachache, asilimia 19.23 walipata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kufafanua vipengele vingi vya fani kwa usahihi. Hata hivyo, asilimia 3.37 walifafanua kwa usahihi vipengele vyote vya fani na kupata alama zote. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kufafanua vipengele vya fani alivyopewa kwa usahihi na kukidhi matakwa ya swali husika.

Kielelezo 8.1

8. Fafanua vipengele vifuatavyo vya fani:

(a) Mandhari.: ni mahali ambapo msanii huamua kazi yake ifanyike. Mahali kama vile mstuni, nyumbani, baharini au vokoni.

(b) Wahusika.: ni wale waifanyaya kazi ya msanii wakiwemo; fanani, hadhira, binadamu, wanyama, vitu na mahali

(c) Fanani.: Ni mtu anayewasilisha kazi ya msanii na kutoa ujumbe uliopo katika kazi ya msanii. mbele ya hadhira kwa nia mbalimbali.

(d) Hadhira.: Ni watu au mtu aupokeao ujumbe aliotoa fanani kwa njia iliyofichika au wazi. Bila hadhira fanani hataweza kutoa ujumbe.

(e) Muundo.: Ni namna kazi ya fasihi ya msanii iliyojengwa: kama vile mashairi, yanamuundo wa shairi huru au mtiririko na shairi la kimapokeo.

Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kufafanua kwa mifano vipengele vya fani katika kazi za fasihi simulizi na kupata alama zote.

Hata hivyo, asilimia 42.02 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kutokana na kushindwa kutoa ufafanuzi unaojitosheleza kwa vipengele vingi vya fani walivyopewa na kupata alama za chini 0 hadi 2.5. Aidha, zaidi ya nusu ya wanafunzi hao, (23.72) walikuwa hawana maarifa mahsusi kuhusu vipengele vya fani katika uhakiki wa kazi za fasihi simulizi na hivyo kupata alama 0. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kufafanua vipengele vyote vya fani kwa kuandika tungo zisizohusiana na ufafanuzi wa vipengele hivyo. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika, “wahusika ni kazi ya fasihi inatumika katika vipera vya

hadithi” kinyume kabisa na maana halisi ya kipengele hicho ambacho hufafanuliwa kama *watendaji katika kazi ya fasihi.*

Kielelezo 8.2


8. Fafanua vipengele vifuatavyo vya fani:

(a) Mandhari. Ni Sehemu nzuri inayo mvutia mtu ndiyo maituwa mandhari

(b) Wahusika. Ni Kazi ya fasihi in tumika katika vipera vya hadithi

(c) Fanani. Ni Kazi ya fasihi anayo pelekewa hadhira.

(d) Hadhira. Ni Kazi ya fanani anayo pelekewa hadhira.

(e) Muundo. Ni maneno au Kitu chenye muundo wake.

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kabisa kufafanua vipengele vyote vya fani kwa kutoa majibu yaliyo kinyume kabisa na matakwa ya swali.

2.4.3 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika kutathmini kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilimtaka mwanafunzi kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi; (a) *Vitendawili na methali*, (b) *Majigambo na ngonjera*, (c) *Misemo na nahau*, (d) *Utenzi na ushairi* na (e) *Michezo ya jukwaani na vichekesho*. Wanafunzi wengi waliojibu swali hili walipata alama za chini na kulifanya swali hili kuwa moja ya maswali yaliyojibiwa vibaya. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi katika asilimia.



Chati Na. 6: *Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia*

Wanafunzi wengi (81.71%) walipata alama za chini 0 hadi 2.5 kutokana na kushindwa kufafanua *kufanana* na *kutofautiana* kwa vipera vya Fasihi Simulizi walivyopewa. Miongoni mwao, asilimia kubwa yaani (62.67%) walipata 0 kwa kuwa walishindwa kabisa kufafanua vipengele vyote, hali inayodhihirisha kuwa wanafunzi hawana maarifa kuhusu mada hii ndogo ya *Vipera vya Fasihi simulizi*. Wanafunzi wengi waliandika maneno tofauti yasiyo na uhusiano wowote na vipera vya fasihi simulizi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika katika vipera karibu vyote maneno haya, "*kufanana kwa rangi isipaswe kushangaa kwani kufanana sikawaida nini kinashangaza* (kufanana) na katika kutofautiana kwa vipera vyote aliandika, "*kutofautiana kwa vitu ni jambo la kawaida kwa mimi nisemavyo usipaswe kushangaa*" majibu ambayo hayahusiani kabisa na kufanana au kutofautiana kwa vipera vya fasihi simulizi alivyopewa. Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali hili kinyume na matakwa ya swali.

Kielelezo 9.1



Eleza kufanana na kutofautiana kwa vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi. Toa hoja moja katika kufanana na hoja moja katika kutofautiana:

(a) Vitendawili na methali

(i) Kufanana: kufana kwa rangi kipaswe kushangaa kwani kufanana sikawaido nini kinawashangaza

(ii) Kutofautiana: kutofautiana kwa vitu vi pamb tokawaida kwa mimi nisemavyo kipaswe kushangaa

(b) Majigambo na ngonjera

(i) Kufanana: kufanana kwa rangi kipaswe kushangaa kwani kufanana sikawaido nini kinawasha-ngaza

Kielelezo 9.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mwanafunzi aliyetoa maelezo ya kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu za fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali.

Hata hivyo, wanafunzi wachache sana, asilimia 18.29 waliweza kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu za fasihi simulizi na kupata alama za wastani na zaidi. Miongoni mwao, asilimia 4.62 pekee ndio waliopata alama za juu 6.5 hadi 10 kwa kuwa waliweza kutoa maelezo ya kutosheleza kuhusu kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu za fasihi simulizi. Idadi hii ndogo ya kiwango cha juu cha kufaulu kwa wanafunzi waliofanya upimaji huu inadhihirisha kuwa, mada kuhusu vipera vya tanzu za fasihi simulizi ilieleweka kwa wanafunzi wachache au haitiliwi mkazo wa kutosha katika ufundishaji na ujifunzaji wake kwa jumla. Aidha, asilimia 13.67 ya wanafunzi walipata alama za wastani 3 hadi 6 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheza katika vipengele vingi. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kueleza kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu za fasihi simulizi kwa

kutoa hoja sahihi japokuwa alikuwa na tatizo la kitahjia kwa baadhi ya maneno kama vile “vitendiwili” badala ya vitendawili.

Kielelezo 9.2

9. Eleza kufanana na kutofautiana kwa vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi. Toa hoja moja katika kufanana na hoja moja katika kutofautiana:

(a) Vitendawili na methali

(i) Kufanana: Vyote ni vipera vya semi ambavyo hutumia lugha ya picha na tamathali mbalimbali za semi ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

(ii) Kutofautiana: Vitendiwili huwasilishwa kama maswali yanayohitaji mtu afikirie ili kupata jibu linalompa ujumbe lakini methali huwa na pande mbili, pande wa kwanza ukionyesha tendo/jumbo/tukio na upande wa pili ukionyesha matokeo ya tendo hilo.

(b) Majigambo na ngonjera

(i) Kufanana: Vyote hi vipera vya maigizo na hivyo vhusisha utendaji wa uitendo mbele ya hadhira ambavyo hufikisha ujumbe uliokusudiwa.

(ii) Kutofautiana: Majigambo ni maigizo yanayoeleza mambo ya kishujaa ambayo mtu au watu walifanya lakini ngonjera ni maigizo yanayohusisha majibizano kati ya pande mbili ambazo muisho huafiki katika jambo moja muishoni.

(c) Misemo na nahau

(i) Kufanana: Vyote ni vipera vya semi ambavyo huwasilisha mawazo fulani katika jamii husika ~~kulingana~~ kwa kutumia lugha ya picha na ya mafumbo.

(ii) Kutofautiana: Misemo ni maneno (vikundi vya maneno) ambayo huwasilisha mawazo au mafundisho fulani kwa watu wa jamii fulani kulingana na desturi zao lakini nabau ni tungo zitumiazo lugha ya picha kuwasilisha ujumbe mfano mkono wa birika = mchoyo (mtoto wa birika umeunganika na mwili wake hivyo hawezi kwingine).

(d) Utenzi na shairi

(i) Kufanana: Vyote ni vipera vya ushairi wenye utenzi mahususi wa maneno na mpangilio maalumu wa silabi kwenye mistari.

(ii) Kutofautiana: Ushairi ni utungo wa ~~lugha~~ kifasihi wenye utenzi mahususi wa maneno, mpangilio maalumu wa silabi na hutumia lugha ya mkato pamoja na mahadhi lakini utenzi ni utungo wenye mpangilio maalumu wa silabi zinazolinganana kila mstari na aghalabu huelezea jambo kwa kirefu.

(e) Michezo ya jukwaani na vichekesho

(i) Kufanana: Vyote ni vipera vya maigizo ambavyo hufikisha ujumbe kwa hadhira vikiambatana na utendaji wa vitendo mbele ya hadhira.

(ii) Kutofautiana: Michezo ya kuigiza ni maigizo ambayo huakisi maisha (jambo) fulani lilitokea (linatokea katika jamii na hutoa suluhisho kama ni tatizo au kuelimisha zaidi juu ya ambo hilo lakini vichekesho ni maigizo yanayowalishwa kwa namna ya ucheshi na kufanya vitendo vinavyoifunza hadhira kwa kuchekesha.

Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetoa maelezo sahihi ya kufanana na kutofautiana kwa vipera vya tanzu za fasihi simulizi kama ilivyotakiwa na kupata alama za juu.

2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI

2.5.1 Swali la 10: Uandishi wa Insha

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika uundaji ambapo mwanafunzi alitakiwa kuandika insha kuhusu "Umuhimu wa Misitu katika Jamii" kwa kutoa hoja nne zisizopungua maneno 150 na zisizozidi maneno 200. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15 na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi ambapo asilimia 79.17 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama za juu 10 hadi 15 na za wastani 4.5 hadi 9.5. Jedwali Na. 4 linaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.

Jedwali Na. 4: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya wanafunzi
0 - 4	101,262	20.83
4.5 - 9.5	188,132	38.7
10 - 15	196,723	40.46
Wengine	29	0.01

Asilimia 40.46 ya wanafunzi waliopata alama za juu waliweza kuandika insha kwa kuzingatia taratibu za uandishi mathalani katika utangulizi waliweza kufafanua 'maana ya misitu'; katika kiini waliweza kutoa hoja nne kuhusu 'umuhimu wa misitu katika jamii' kama vile *vyanzo vya mvua, vyanzo vya maji, kutupatia mbao, hewa safi, kuni/mkaa, kuzuia mmonyoko wa ardhi* na nyinginezo. Wanafunzi hao walifafanua vizuri hoja walizotoa na kutoa hitimisho zuri lililoendana na hoja zilizotolewa. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyekidhi vigezo vya uandishi wa insha kuhusu umuhimu wa misitu katika jamii na kupata alama za juu.

Kielelezo 10.1

UMUHIMU WA MISITU

Misitu ni mkusanyiko wa miti ambayo hukua katika eneo moja. Miti hiyo yaweza kuwa ya kupandwa au kukua yenyewe. Umuhimu wa misitu katika jamii nikama ifuatayo:-

Ni chanzo cha mvua. Misitu huchukua sehemu ya pekee katika mvua kwa kuwa hutoa mvuke ambao ukipoa hutengeneza mawingu ambayo baadae hunyesha kama mvua katika eneo hilo na jamii hupata maji.

Misitu ni chanzo cha kuni na mbao. Baadhi ya miti katika misitu hufaa kwa mbao ambazo



hutumika katika ujengaji na shughuli mbali mbali, vilevile baadhi ya miti hutumika kama kuni. ambazo ni chanzo cha kuwachia moto kwa shughuli mbalimbali kama vile kupika.

Misitu huzuia mmomonyoko wa ardhi. Hali hii husababishwa pale ardhi inapoachwa wazi hivo humomonyoka lakini katika misitu, ardhi, hile huepushwa na momonyoko kwa kuwa miti yazuia maji kuharibu sehemu ya juu ya ardhi.

Ni chanzo cha matunda na dawa. Baadhi ya miti hutoa matunda ambayo yawoza kuliwa na wanajamii na mengine hutumika kama dawa kutoka kwenye mizizi au majani yake. Kwa mfano mwarobaini.

Hivyo basi, ni vyema wanajamii kutunza misitu na vilevile kupanda miti kwa wingi. katika kutunza misitu, watu wanahimizwa kutokukata miti ovyo ili misitu iendelee kuwepo katika vizazi vijavyo.

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika insha ya hoja kwa kufuata taratibu zote na kufafanua umuhimu wa misitu katika jamii kama ilivyotakiwa.

Hata hivyo, asilimia 38.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu kwa kupata alama 4.5 hadi 9.5 kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza na wengine wakitoa utangulizi au hitimisho lisilolingana na matakwa ya swali au kutozingatia taratibu za uandishi wa insha. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alielezea umuhimu wa misitu kwa kutoa hoja dhaifu na zisizozingatia idadi stahiki ya maneno na taratibu za uandishi kama vile *mpangilio wa aya* na *mpango wa mawazo wenye mantiki* na kupata alama za wastani kama kielelezo 10.2 kinavyojidhihirisha.

Kielelezo 10.2



UMUHIMU WA MISITU

Misitu ni kitendo cha kujikusanya
miti sehemu moja kuna umuhimu
mwingi sana wa misitu nazo
ni kutupatia mbao kwa ajili
ya kujengea nyumba misitu ni
chanzo cha mvua endapo sehemu
haina misitu basi kutakuwa na
uhaba mkubwa wa mvua watu
wengi sana hapa nchini wanakuwa
wakalibifu wa misitu kukata tu
miti kihotela hivyo hutasababisha uhaba
wa misitu katika jamii utegemea
miti kwa ajili ya kuni.
mkaa misitu mingi sana inakifachi
wanyama pori mfano simba, chui
ngamia, sungura, tembo na wengineo
Misitu inatupatia fedha kwa rahisi
kwasababu miti inajiotesha wenyewe katika
eneo fulani wewe ni nguvu
zako tu kwenda kukata miti
na kukatisha mbao na kuuza
na kujipatia fedha kujikimu maisha



misitu utumika katika kutupatia hewa
ya oksigeni na kuweza kuishi
misitu ukikatishwa mbao utumika kuta
madirisha na milango meza makabati vi
kwa asilimia mia hapa nchini
mbao ni muhimu sana hapa
kwasababu kutupatia fedha, mbao, mamai
Misitu ni muhimu sana tuitunze
ili nayo iweze kututunza pia

Kielelezo 10.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika insha isiyojitoleza kwa *hoja, idadi ya maneno, kutopanga hoja katika aya* na *kutozingatia mawazo yenye mantiki*. Hata hivyo mwanafunzi huyu alikuwa na tatizo kubwa la kisarufi na la kitahijia kama alivyoandika “kuhalibika” badala ya kuharibika, “oksigeni” badala ya oksijeni na makosa mengine mengi ya kisarufi.

Wanafunzi wachache, asilimia 20.83 walishindwa kuandika insha kutokana na kukosa maarifa na mbinu za uandishi na kufaulu kwa kiwango cha chini kuanzia alama 0 hadi 4. Miongoni mwao, asilimia 6.72 walishindwa kabisa kuandika insha na kupata alama 0 kwa kuandika mambo tofauti kabisa na insha iliyotakiwa. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walichanganya dhana ya uandishi wa insha na *utunzi wa shairi*; *uandishi wa barua* na wengine *walitunga hadithi* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 10. 3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika 'barua rasmi' kuhusu umuhimu wa misitu katika jamii badala ya 'insha' kama ilivyotakiwa.

Kielelezo 10.3


10. Kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200, andika insha kuhusu Umuhimu wa Misitu katika Jamii kwa kutumia hoja nne.

Juma Simoni Haonga
S.L.P 388
Moshi
22/8/2003

Ndugu
YAH: UMUHIMU WA MISITU KATIKA JAMII
Husika na kichwa cha habari hapo juu mimi ni kijana mwenye umri wa miaka 28. Sijaoa. Nafanda Kusema kwa kua misiti ni muhimu sana katika maisha ya viumbehai faida za kuwa na misitu ni kuwa pa la nyumba kwaka pia tunapata hewa nzuri, pia tunapata mbao, pia tunapata kuni hata na mkaa.

Kielelezo 10.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika barua rasmi na inayoelezea umuhimu wa misitu lakini hakuweza kupata alama yoyote kwa kuwa hakuzingatia muundo wa insha.

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KATIKA MADA

Kiwango cha kufaulu katika mada kwa mwaka 2017 kimeshuka katika mada nyingi ikilinganishwa na mwaka 2016. Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa, wanafunzi wengi walifaulu kwa kiwango cha wastani katika mada nyingi kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo wanafunzi walifaulu kwa kiwango cha juu (kizuri) katika mada zote. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, katika upimaji wa somo la Kiswahili kwa mwaka 2017, mada za *Utungaji na Ufahamu* zilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu ambapo katika mada ya *Utungaji* (79.17%) ilikuwa na ongezeko la asilimia 0.67 ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2016 na mada ya *Ufahamu* (72.45%) ikiwa imepungua kwa asilimia 5.05 ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2016. Hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kutokana na ufundishaji na ujifunzaji mzuri wa dhana mbalimbali kuhusu mada hizo (*Utungaji na Ufahamu*).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, mada nyingine zote zilikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo mada ya *Fasihi Simulizi* ilikuwa na kiwango cha kufaulu cha asilimia 56.82, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (55.35%) na *Sarufi* (50.81%). Kwa jumla, wastani wa kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika mada zote ni asilimia 62.92, kiwango ambacho ni cha chini kwa asilimia 14.58 ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kwa mada zote kilikuwa (77.5%). Kiwango hiki cha kufaulu kinaashiria kuwa wanafunzi wengi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika na hivyo kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa maswali mengi.

Kwa jumla, kiwango cha kufaulu cha wanafunzi kimeshuka kwa mada nyingi ilikinganishwa na kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2016 ambapo mada ya *Sarufi* imekuwa na kiwango cha chini zaidi kutokana na wanafunzi wengi kukosa maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu kazi mbalimbali za mofimu katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, mada zote zilizokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu yaani *Fasihi Simulizi*, *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* na *Sarufi* zinatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wake ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa na kuwafanya kuwa mahiri katika somo la Kiswahili na hatimaye kuongeza kiwango cha kufaulu katika mada zote.

Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika mada mbalimbali kwa mwaka 2017 kimeainishwa katika **Kiambatisho A**. Pia ulinganifu wa viwango vya kufaulu vya wanafunzi katika mada kwa mwaka 2016 na 2017 umeainishwa katika **Kiambatisho B.**

4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2017 katika somo la Kiswahili ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia majazi ya utambuzi (*maarifa, ufahamu, utumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini*). Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi kilikuwa kizuri ambapo wastani wa kufaulu kwa jumla ulikuwa ni asilimia **91.92**.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali kama vile, wanafunzi wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizopimwa kama vile, *Sarufi, Fasihi Simulizi* na *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*. Aidha, wanafunzi wengine walishindwa kufuata maelekezo ya maswali ipasavyo. Changamoto hizo hazina budi kutatuliwa ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili. Utatuzi wa baadhi ya changamoto ni pamoja na kusisitiza matumizi ya lugha sanifu na fasaha ili kuondokana na tatizo la makosa ya kisarufi katika mawasiliano kwa jumla. Aidha, wanafunzi sharti wapatiwe mazoezi ya kutosha ya kisarufi ili kuwajengea weledi katika mada ya Sarufi. Pia, ili kukabiliana na changamoto za kifasihi (Fasihi Simulizi) wanafunzi wapewe mazoezi ya kusimulia hadithi na kutunga kazi mbalimbali za fasihi simulizi kama vile vitendawili, methali, nahau, misemo, hadithi na nyinginezo ili kuwajengea ujuzi wa kuweza kutunga na kuendeleza kazi mbalimbali za fasihi simulizi. Licha ya hayo, jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa jumla ili kuwajengea wanafunzi uwezo na ujuzi wa kutumia lugha katika stadi zote nne za lugha yaani *kusikiliza, kuzungumza, kuandika* na *kusoma* ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa.

Aidha, Uchambuzi huu unaonesha pia kuwa, zipo mada zinazohitaji jitihada za dhati katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii ni kwa sababu viwango vya kufaulu vya mada hizo vimeshuka kwa muachano wa asilimia kubwa kutoka viwango vizuri vya mwaka 2016 na kuwa vya wastani kwa mwaka 2017 isivyotarajiwa. Kwa mfano, kiwango cha kufaulu kwa mada ya *Sarufi* (50.81%) kimeshuka kwa asilimia 35.39 kutoka asilimia 86.2, *Mawasiliano*

na Utumizi wa Lugha (55.35%) kimeshuka kwa asilimia 40.95% kutoka asilimia 96.3 na *Fasihi Simulizi* kimeshuka kwa asilimia 23.08 kutoka asilimia 79.9.

Mwisho, taarifa hii ya upimaji kuhusu uchambuzi wa majibu ya wanafunzi inatarajiwa kuwa chachu ya mabadiliko kutoka kiwango cha wastani cha kufaulu na kuwa kiwango kizuri cha kufaulu katika mada mbalimbali za somo la Kiswahili. Aidha, hii ni njia mojawapo ya utatuzi wa changamoto kwa walimu na wanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali na kuelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kiwango cha kufaulu kuwa cha chini kwa baadhi ya mada kwa lengo la kuinua kiwango hicho kipindi kijacho.

MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

(a) Walimu wasisitize wanafunzi kutilia mkazo katika kujifunza mada za *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha, Sarufi* na *Fasihi Simulizi* (uhakiki wa vipengele vya fani) kwani ni mada ambazo wanafunzi wameonesha uwezo mdogo wa kuelewa katika kujibu maswali husika.

(b) Serikali iendelee kutoa semina elekezi kwa walimu waliopo kazini ili kuwajengea uwezo zaidi katika ufundishaji wa mada mbalimbali za somo la Kiswahili ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi.

(c) Serikali na wadau wa elimu kwa jumla waweke na kusimamia matumizi ya vitabu vya kiada vinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za sekondari nchini Tanzania.

(d) Matumizi ya lugha fasaha ya Kiswahili yasisitizwe kwa wanafunzi katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuongeza umahiri katika lugha ya Kiswahili.

(e) Walimu wasisitize wanafunzi kusoma vitabu vya kiada na ziada na matini mbalimbali za lugha ya Kiswahili ili kuwajengea umahiri katika stadi za kusoma na kuandika.

KIAMBATISHO A

UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA KWA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2017

Na	Mada	Idadi ya Swali	Asilimia ya Wanafunzi waliopata wastani wa asilimia 30 au zaidi	Maoni
	Uandishi wa Insha/Utungaji	10	79.17	Vizuri
	Ufahamu.	1 na 2	72.45	Vizuri
	Fasihi simulizi	7, 8 na 9	56.82	Wastani
	Mawasiliano na Utumizi wa Lugha	5 na 6	55.35	Wastani
	Sarufi	3 na 4	50.81	Wastani

KIAMBATISHO B

ULINGANIFU WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2016/2017